HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA MHESHIMIWA HAWA A. GHASIA, MB. KATIKA UFUNGUZI WA SEMINA ELEKEZI YA WADAU WA MPANGO WA 'KiuFunza' DAR ES SALAAM, 23 JANUARI 2013

Waheshimiwa Wabunge,
Wawakilishi wa Wadau wa Elimu,
Makatibu Wakuu,
Makatibu Tawala Mikoa,
Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri Nchini,
Wakuu wa Mashirika mbalimbali,
Wanazuoni wetu,
Washiriki wote,
Mabibi na Mabwana;
Asalaamu Aleykum.

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia wote afya njema hata kutuwezesha kuhudhuria Semina hii.

Ninayo furaha kubwa leo hii kukutana nanyi nyote katika hafla hii ya ufunguzi wa Semina elekezi ya mpango wa Kuitafiti Elimu ujulikanao kama '**KiuFunza'**. Malengo ya mradi huu ni kupata ufumbuzi wa changamoto muhimu ambazo zinaikabili Nchi yetu katika kutoa elimu kwa watoto na vijana wetu.

Waheshimiwa Wabunge na Washiriki wote,

Kama mjuavyo, elimu ndio msingi wa maendeleo ya jamii yoyote ile. Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere baada ya Tanganyika kupata uhuru aliiona elimu kama chombo cha kuikomboa nchi na Bara la Afrika kwa ujumla. Leo hii, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete pia anatambua ukweli huo na kwa sababu hiyo amekua mstari wa mbele katika kupanua fursa za elimu kwa ngazi zote. Umuhimu wa elimu katika kumkomboa binadamu umedhihirishwa pia katika matokeo ya tafiti mbalimbali za Kimataifa; kwamba jamii iliyoelimika huwa na watu wenye afya na maisha yenye ubora. Hivyo, Elimu ndio injini madhubuti ya kuifikisha jamii kwenye kilele cha maendeleo. Kwa kufahamu umuhimu wake, suala la elimu limezingatiwa na kujumuishwa katika Sera zetu zote kama 'Dira ya Maendeleo na hata MKUKUTA.

Ndugu Washiriki,

Kwa kuwa Elimu ni muhimu katika kuchochea maendeleo, katika muongo uliopita, Tanzania imewekeza na kutenga rasilimali nyingi katika elimu. Kwa mfano, utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi (MMEM.). Jambo la kujivunia ni kuwa tumeweza pia kufikia uwiano sawa kati ya watoto wa kike na kiume. Mafanikio haya yameifanya Nchi yetu iwe na

mwelekeo wa kutekeleza kwa ufanisi Malengo ya Maendeleo ya Milenia katika Elimu mafanikio ambayo yameiletea Nchi yetu sifa Ulimwenguni kote.

Ndugu Washiriki,

Hata hivyo, mafanikio yote haya yamekuja na changamoto zake. Hivyo basi, changamoto tulizonazo hivi sasa sio wingi wa wanafunzi walio shuleni bali kutoa **Elimu Bora kwa Wote**, yaani watoto na vijana wote walioko shuleni. Mafanikio tuliyopata katika kupanua fursa za elimu yatapotea endapo wanaohitimu katika ngazi yoyote watakuwa hawana stadi na maarifa wanayohitaji kwa ajili ya maisha yao, ajira au kujiajiri. Kwa hiyo tunalazimika hivi sasa kutafuta mbinu na taratibu za kiutendaji ambazo zitachochea kujifunza na kupata elimu iliyo kamilifu.

Ndugu Washiriki,

Semina hii ni muhimu kwa kuwa lengo lake ni kutafiti ili zipatikane mbinu na taratibu za kiutendaji zitakazoleta ufanisi katika kufundisha na kujifunza. Kwa maelezo ya kina zaidi ni kwamba;

Kwanza, utafiti utakaofanywa chini ya mpango huu wa **'KiuFunza'** unalenga kuona matokeo ya kujifunza na sio kuwekeza katika elimu tu bila kujali ubora.

Serikali hivi sasa inaondokana na mtazamo wa kupima matokeo ya elimu kwa vigezo vya idadi ya uandikishaji, idadi ya madarasa, walimu au vitabu, kiasi cha fedha zilizotengwa katika bajeti ya elimu n.k. Kuanzia sasa tunataka kuwa na vigezo halisi zaidi vya kupima mafanikio ya uwekezaji kwa kudadisi je, idadi gani ya watoto wanapata stadi za kudumu za kusoma, kuandika na kuhesabu, sayansi n.k.? Tunataka kufahamu viwango vya stadi walizopata zitakazowezesha na kuendesha uchumi wetu.

Lengo kuu chini ya mpango huu wa **'KiuFunza'** ni kwamba; tufanye nini ili watoto waweze kukuza stadi za kusoma na kuhesabu katika darasa la Kwanza hadi la Tatu; kwani huu ndio msingi madhubuti wa elimu kwa kuwa ni kweli mtoto hawezi kukimbia kabla ya kutambaa; wala nyumba haiwezi kuezekwa kabla msingi haujajengwa.

Ndugu Washiriki,

Jambo kuu katika utafiti utakaofanywa chini ya mpango huu wa **'KiuFunza'** ni kupata njia mbadala kwa kutumia mawazo mawili makuu. Kwanza ni kutafiti juu ya taratibu muafaka za kutoa kiwango cha fedha za uendeshaji wa shule ya msingi "CG" kwa muda unaotakiwa na kwa uwazi zaidi na pili; jinsi ya kuwamotisha walimu pale ufundishaji wao unapowezesha watoto kujifunza kwa ufanisi kuliko ilivyo sasa – yaani 'cash on delivery'.

Napenda kueleza kuwa wazo hili la motisha au bahshishi ni jipya hapa nchini, yaani – kumpa mwalimu bahshishi kulingana na matokeo ya kazi ya kufundisha. Nieleze hapa kwamba, wazo hili limetokana na mawazo ambayo Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete aliyapata

alipoitembelea Taasisi ya Maendeleo ya "*Center for Global Development*" huko Marekani. Tafiti zilizofanywa na Taasisi hii kwingineko Duniani zimeonesha kuwa kuna ongezeko kubwa la ufanisi pale mwalimu anapopewa bahshishi kwa kazi na matokeo mazuri ya wanafunzi wake. Alipenda na kuagiza wazo hili lifanyiwe kazi na *Twaweza* ikaagizwa kulifanyia majaribio. Hivyo, ninafurahi kuona kuwa mawazo ya Rais yatajumuishwa na kufanyiwa majaribio hapa Tanzania kwani hapo nyuma mawazo ya kuwamotisha wanaofanyakazi ngumu au katika mazingira magumu hayajawahi kutekelezwa.

Nachukua fursa hii kuipongeza *Twaweza* na washirika wake kwani kazi wanayoifanya sasa sio kuonesha mapungufu yaliyopo katika elimu yetu tu bali sasa wanasaidia katika kutafuta ufumbuzi wa mapungufu hayo.

Suala la kuwa wabunifu ni lina umuhimu wa kipekee katika mambo ya elimu. Watendaji katika Sekta hii lazima wawe tayari kupokea mawazo mapya. Hatuwezi kuongeza ubora wa elimu kwa kutegemea au kutumia taratibu na mbinu zilizile ambazo zimetumika kwa miaka 40 iliyopita la hasha, Dunia sasa imebadilika, zimezuka changamoto mpya, na zipo pia fursa mpya. Upo ushahidi wa kisayansi kuhusu mbinu ambazo zimeleta mafanikio mahali pengine Duniani; Je hizi zinaweza kutumika hapa Tanzania.

Ndugu Washiriki,

Katika kutafuta ufumbuzi wa matatizo makubwa kama haya ya kielimu, lazima pia tuangalie thamani ya uwekezaji wetu. Je, uwekezaji huo umekuwa na matokeo gani? Ninatumaini kuwa tafiti zitakazofanywa zitatoa ushahidi kuhusu mambo ambayo yataleta ubora katika elimu ili uamuzi wa kisera na kiutendaji uwe na tija na uwe wa nafuu kifedha.

Ninapata faraja kuona kuwa mpango huu utatumia njia za kisasa na za kisayansi chini ya usimamizi wa Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH), na kwa kushirikiana na "*Poverty Action Lab at MIT*". Hivyo basi, lengo la mpango huu la kupata ushahidi wa kuaminika kisayansi ni ili Sera zilingane na uhalisia wa kiutendaji na manufaa yake. Katika karne hii ya 21 hatuwezi kufanikiwa kama hatutatumia mbinu za kisayansi katika kupata ufumbuzi wa masuala ya kijamii na kwamba sera zetu zilenge pia katika matumizi ya rasilimali zetu kwa kuleta tija.

Mpango huu wa **'KiuFunza'** utatumia mbinu ya majaribio iitwayo 'Randomized Control Trial (RCT), mbinu ambayo huwapata washiriki kwa njia ya bahati nasibu ambapo jumla ya Wilaya 11 zilipatikana na ndizo Wilaya zinazofanyiwa majaribio.

Ndugu Washiriki,

Mwisho, kama inavyotegemewa Serikali iko tayari kupokea mawazo mapya yatokanayo na ushahidi wa kisayansi. Hivyo, ninaamini utekelezaji wa mradi huu utakuwa wa wazi pia. Fanyeni mawasiliano na Mikoa, Halmashauri na Shule zitakazochaguliwa kwa uwazi na pia kutoa taarifa za jinsi kazi inavyoendelea. Ninaamini pia kuwa mtafanya majumuisho ya matokeo ya utafiti

huu kwa uwazi pia ili watunga sera waweze kutumia matokeo hayo kuandaa sera na mipango itakayokuwa na tija kielimu.

Nawashukuru sana *Twaweza* na washirika wake wote, ninawatakia mafanikio mema katika shughuli zenu za kila siku.

Baada ya kusema maneno hayo ya utangulizi, napenda kuwa Semina hii imefunguliwa rasmi.

Asanteni sana kwa kunisikiliza.